## SURA YA KWANZA

## MTOTO NA MALEZI

***Zaburi 127:3, Tazama wana ndio urithi wa BWANA, Uzao wa tumbo ni thawabu,4,kama mishale mkononi mwa shujaa,Ndivyo walivyo wana wa ujanani,5,Heri mtu Yule Alielijaza podo lake hivyo Naam,hawataona aibu Wanaposema na adui langoni.***

Watoto ni thawabu na Baraka kutoka kwa Mungu, ni urithi wa Mungu,ni hazina ya dunia,ni mishale ya wazazi na thawabu. Baraka na hazina hii inahitajika kutunzwa kwa bidii na umakini mkubwa kwa kujenga msingi imara katika Neno la Mungu ili makusudi ya Mungu yatimie katika maisha ya watoto wetu.Kinyume cha hili ni matatizo makubwa.Ili tuweze kutimiza kusudi jema la Mungu la kuwafanya watoto wawe baraka na kuishi maisha ya kumcha Mungu, kuupata wokovu na kisha uzima wa milele kama yalivyo makusudi ya Mungu ni lazima yawepo maandalizi na mipango madhubuti katika malezi pasipo kulegea na kujisahau.Neno la Mungu linatuelekeza kufanya jambo hili kwa bidii likionesha umuhimu na ulazima wa kufanya hivi siku zote kwa watoto wetu.

Twaweza kujiuliza maswali mengi wakati wa Kujifunza masomo haya ya malezi ya watoto, lakini kabla ya kuanza safari yetu ya kujifunza na tujiulize swali hili kwa makusudi ya kujifunza.

***Kwanini tuwalee watoto kwa bidii katika msingi wa na neno la Mungu? Biblia inatufundisha yafuatayo:-***

1. Ni Agizo la Mungu kwa wazazi/Walezi. ***Mithali 22:6.***
2. Watoto Ni Moyo wa Mungu .***Mathayo 18:2-3.***
3. Watoto ni thawabu (ni utukufu wa Mungu)
4. Watoto ni adimu. (rasilimali adimu haipatikani kirahisi)
5. Watoto ni Baraka.***Mwanzo 48:9***.
6. Ni haki ya watoto kutunzwa na kulelewa.
7. Watoto ni hazina na urithi wa Mungu, Wazazi Na Ulimwengu.
8. Watoto ni Utajiri tunaopewa na Mungu.
9. Watoto waufikie wokovu (hivyo ni lazima wafundishwe, walelewe katika msingi imara).

10. Watoto wanawindwa na shetani (lazima wafundishwe Neno la Mungu ili walindwe na uharibifu).
11. Lazima wamjue Mungu Kama wazazi wao.
12. Watoto ni mishale mikononi mwa wazazi ni fahari ya Wazazi ni silaha ya wazazi. -***Zaburi 127:3-5.***

**A. MTOTO NI NANI?**

Mtoto anatafsiriwa kwa namna mbalimbali kulingana na eneo husika la kitaalamu, umri na hatua za ukuaji.Wanasheria,wanaharakati wa maendeleo ya jamii,wanasiasa na mashirika mbalimbali ya umoja wa mataifa wamemwelezea mtoto na kumtambulisha kwa kusudi la kulea,kukuza,kulinda haki za watoto,na kutoa huduma stahiki kwa watoto.

**Biblia** imetoa ufafanuzi mzuri sana kuhusu Mtoto kwa mifano mingi kuonesha malezi ya mtoto katika neno la Mungu katika hatua zote za ukuaji wa Mwanadamu.

**Taaluma**

**Sheria**, hutueleza kuwa mtoto ni mtu aliye chini ya miaka 18 na pale sheria itakapofafanua kiundani kulingana na mazingira yake na sheria ya mahali fulani ama nchi husika.

**Unicef**, wanatueleza kuwa mtoto ni Yule mtu mwenye umri ulio chini ya umri uliokubaliwa na wengi kuwa wa watu wazima (Age of majority, below 18 years).

Unicef wamejitahidi sana kumuelezea mtoto na kuanzisha sheria mbalimbali kwa ajili ya malezi na makuzi ya watoto duniani kote, kama sheria hizi hapa chini:-

1. Convention on the Rights of the child

2. African charter on the rights and welfare of the child

**Matabibu (Madaktari)**, (biologically) wanamweleza mtoto kibaolojia kuwa, mtoto ni kati ya umri wa miaka sifuri (0) mpaka kufikia umri wa kupevuka (puberty period), ama kwa kiingereza inasemwa kuwa (the period in which the human body first becomes capable of reproduction).Pale mwili wa mtoto unapopata sifa za mtu mzima yaani kuweza kufanya mambo ya watu wazima kama kuzaa, nk.

**Sayansi ya jamii (Sociology)**, wao hutueleza kuwa mtoto ni kipindi kile ambacho mtu hajafikia kubeba majukumu katika jamii yake, kama kuoa, kupiga kura,

kupigiwa kura na kupewa nguvu ya kufanya maamuzi katika jamii kulingana na mila, desturi na sheria za inchi aliyopo.

**Kamusi kuu ya Kiswahili KKK (2017)**

Inasema mtoto ni mwanadamu mwenye umri mdogo ambaye bado hajafikisha umri wa kubalehe.

**Maelekezo ya Biblia**

Biblia,Imetoa maelezo ya kutosha na makini sana yanayomuelezea mtoto.Biblia imekwenda mbali zaidi ya wanataaluma wa ulimwengu na kumuelezea mtoto na malezi ya misingi ya kiroho katika malezi kuanzia matayarisho (ujauzito), kuzaliwa,kukua, utu uzima,uzee, kifo na uzima wa milele.Biblia imetueleza pia utoto kwa namna ya **rohoni.**

**Namna Tofauti tofauti, (Figulatevely) Ya Maelezo Ya Mtoto Katika Biblia**

Lazima tujue kwanza Biblia inapozungumzia neno mtoto inamaana zaidi ya moja kulingana na maudhui ya mlango husika.Hii inaifanya biblia kwenda ndani zaidi ya wanataaluma walivyoeleza awali kuhusu mtoto ambao wameeleza upande wa mwili tu kuhusu mtoto, kwa maana hii biblia ni tajiri wa mafunzo makubwa kwa wazazi na ulimwengu dhidi ya wataalamu wa ujuzi mbalimbali wa dunia kuhusu malezi ya mtoto.

Tazama biblia inavyoeleza kuhusu mtoto katika maandiko yafuatayo iili tujifunze:-

**Mtoto Wa Kimwili**-(biological child) mtoto wa kuzaa kwa namna ya mwili.

***Luka 1:57, Ikawa siku ya kuzaa kwake Elisabeth zilipotimia, alizaa mtoto mwanamume***.

**Mtoto Wa Kiroho** (Sons of God) mtu aliezaliwa mara ya pili kwa maana ya kuupata wokovu.

***Yohana 1:12-13 Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu,Ndio wale waliaminio jina lake,waliozaliwa,si kwa damu,wala si kwa mapenzi ya mwili,wala si kwa mapenzi ya mtu,bali kwa Mungu.***

***2Wakorithno 6:18 Nitakua Baba kwenu, Nanyi wanangu wa kiume na wa kike asema Bwana Mwenyenzi.***

**Mtoto Kiroho**,Ni mtu asielifahamu neno sahihi la Mungu,Mtu asiyejua Neno la Mungu, **spiritual narrow minded person**, aliepotoka, ajuae dhambi zaidi kuliko kumjua Mungu na neno lake.Mchanga kiroho, wasio na msimamo katika imani, wanaodanganywa kirahisi na mafundisho ya uongo na asiekuwa kiroho.(wakati mwingine mwongofu mpya huitwa mtoto kiroho).

***1Wakorithno 13:11 Nilipokua mtoto mchanga, nalisema kama mtoto mchanga, nalifahamu kama mtoto mchanga, nalifikiri kama mtoto mchanga, tokea hapo nilipokua mtu mzima nimeyabatilisha mambo ya kitoto.***

***Waefeso 4:14 Ili tusiwe WATOTO wachanga tukitupwatupwa huku na huku na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu kwa hila ya watu kwa ujanja tukizifuata njia za udanganyifu.***

***1Wakorithno 14:20 Ndugu zangu, msiwe watoto katika akili zenu, lakini katika uovu mgeuzwe watoto wachanga, bali akili zenu mkawe watu wazima.***

**Majumuisho Ya Biblia Kwa Ufupi**

***Biblia imetufafanulia namna mbili za Mtoto,moja kwa maana ya kuzaa kimwili na mbili watoto katika namna ya roho yaani uchanga kiroho.Katika kitabu chetu tutajifunza malezi ya mtoto wa kimwili yaani watoto tunaowazaa.***

Biblia imemuelezea mtoto na kumtafsiri kuwa ni mtu/mwanadamu katika hatua mbalimbali za ukuaji kwa kumueleza kabla (ujauzito) na baadae kuzaliwa na kuwa ni nafsi na roho iliyo hai ambayo Mungu ameiumba kwa pumzi yake na kuiruhusu ije duniani kupitia mwanamke,mtu huyu ama nafsi hii inaanzia katika wazo, na mpango wa Mungu kumuumba mtu fulani,baadae mimba na hatimaye mtoto aliyezaliwa na hupitia hatua mbalimbali za ukuaji wa binadamu hata kufikia utu uzima na mwisho kifo na uzima wa milele kama maandiko yanavyoonesha.

***Yeremiah 5:1 Neno la Bwana lilinijia, kusema, kabla sijakuumba katika tumbo nalikujua,na kabla hujatoka tumboni nalikutakasa,nimekuweka kuwa nabii wa mataifa.***

Fahamu ya kuwa mtoto wako kabla hujamzaa Mungu alimfahamu na kumuandaa,na fahamu kuwa Mungu amekuheshimu kukupa nafasi ufanyike mzazi wa huyo mtoto hivyo tunza dhamana hii uliopewa kwa uaminifu na hofu ukijua kuwa Mungu atakuuliza kwa namna ulivyomlea,kama uliwajibika kuweka msingi imara wa Neno la Mungu ili akaue kwa mafanikio na kumjua Mungu.

**B.MALEZI NI NINI?**

Malezi ni utunzaji, ukuzaji, uangalizi, ufunzaji wa kiina wa mzazi/mlezi kwa mtoto katika maeneo yote ya maisha yake yaani kimwili, kiroho kiafya,kielimu na kiakili ili kumfikisha mtoto kwenye uwezo wa kujitambua,kupambanua mambo na kujiendesha mwenyewe kama mwanadamu kamili.

Malezi ni kazi inayostahili moyo mkuu na ustahimilivu kwakuwa ni kazi ngumu na ya dhamana kubwa.

***Mithali 22:6, Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataicha hata atakapokua mzee.***